HALMASHAURI YA MJI HANDENI

SHULE YA SEKONDARI MISIMA,
S. L. P 192,
HANDENI.
MOB: 0755015247/ 0677671520.
15/12/2020.

Kumb Na. **MSS/A/Vol/1/16**
Jina la Mwanafunzi .....

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 SHULE YA SEKONDARI MISIMA.

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2021 katika shule hii nimatumaini yangu utaitumia nafasi hii vizuri. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 hivyo ufike siku hiyo saa 1:00 asubuhi bila kukosa.

1.0. MZAZI

(i) Muandae mwanao vizuri ili aweze kusoma na kupata mafanikio. Kama utampangishia chumba mwanao, kwa wale wanaotoka mbali ni vyema uhakikishe usalama wa sehemu hiyo uweke uwangalizi wa karibu vinginevyo utaingia hasara. Usifanye kosa la kumuamini mwanao kwa asilimia mia.

(ii) Hakikisha unamtengenezea mwanao **kiti** na **meza** na aje navyo siku ya kuripoti shuleni vinginevyo mwanao atakaa chini.

(iii) Mnunulie begi la shule, kaunta buku 10, mkebe wa Hisabati na kalamu za kutosha.

2.0. SARE ZA SHULE

Sare za shule hii ni shati jeupe mikono mifupi, soksi nyeupe na viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba kwa wavulana na wasichana.

2.1. Wavulana washone suruali za kitambaa rangi ya kaki mshono wa kawaida wenye marinda.

2.2. Wasichana washone sketi ndefu zenye rinda 8 hadi 10. Kila sare pea mbili. Wanaotaka kuvaa hijabu wanapaswa kushona suruali pana, kanzu fupi na kitambaa cheupe kisichokuwa na mapambo.

2.3. Kila mwanafunzi anuniliwe raba za michezo na Bukta.
Fulana (T-shet) za shule zinapatikana kwa Tsh 10,000/=.

2.4. Mashati yatawekwa nembo ya shule kwa gharama ya Tsh 2,000/= tu hivyo aje nayo siku ya kuripoti shuleni.

2.5.Sweta rangi ya darkblue

3.0. Mwanafunzi aje na fagio la chelewa kwa ajili ya usafi wa kila siku.

4.0. Siku ya kuripoti mwanafunzi aje na kwanja au fyekeo kwa ajili ya usafi wa maeneo ya nje.

4.1. Kutokana na uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi wazazi walikubaliana katika kikao chao cha February 2020 kila mwanafunzi achangie Tsh 8,000/= kuajiri Walimu Wawili (2). Hivyo mwanafunzi aje na hela hiyo siku ya kuripoti shuleni. Ambapo kila Muhula ni Tsh 4,000/=.

4.2. Kila mwanafunzi aletwe na chakula cha mchana ambacho ni kilo 25kg za sembe, kilo 12 za maharage, na pesa 10,000/= ni gharama za mpishi na mafuta ya kupikia kwa nusu mwaka.
Haya yote hulipwa mwanzo wa Muhula shule inapofunguliwa Januari na Julai.

4.3. Mwanafunzi lazima apimwe afya yake na Mganga (HOSPITALI) anayetambulika na Mhuri ugongwe panapohusika, fomu kwa ajili ya shughuli hiyo imeambatanishwa.

5.0. TAARIFA YA MAENDELEO

Kila inapofungwa shule hakikisha mwano anakupa ripoti ya maendeleo ili wewe upate nafasi ya kumshauri kimaadili na kitaaluma.

6.0. SHERIA ZA SHULE

Baadhi ya sheria muhimu za shule zimeambatanishwa na mwanao anaagizwa kuzisoma na kuzizingatia ili asome bila shida.

SHERIA ZA SHULE:

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

(a) Uasherati na Ushoga
(b) Ubakaji
(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya. Kama vile uvutaji wa bangi, cocein mirungi, kuberi na kadhalika.
(d) Wizi
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Shule (UMMA)
(g) Kudharau Bendera na Wimbo wa Taifa
(h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kutia mimba
(i) Kutoa mimba.
(j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(l) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule au line ya simu. Ni marufuku mwanafunzi wa shule hii kuwa na simu ya mkononi. Mawasiliano kati ya wazazi/mlezi yatafanyika kupitia ofisi ya mkuu wa shule au mwalimu aliyekaimishwa.
(m) Kutohudhuria vipindi vya darasani bila ya taarifa
(n) Kutofanya kazi za darasani na nje ya darasa.
(o) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kuua au kujiua kama kunywa sumu n.k.

MKUU WA SHU
MISIMA SEKONDA
HANDENI

.....

MKUU WA SHULE
MISIMA SEKONDARI

HALMASHAURI YA MJI – HANDENI
SHULE YA SEKONDARI MISIMA
S. L. P 192
HANDENI

TAMKO LA MZAZI

Mimi……..(Jina la Mzazi/Mlezi) wa mwanafunzi…….. Nakubali/Sikubali mwanangu ajiunge kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Misima kwa sababu
……
……
……

Nimesoma maelezo yote katika barua ya kujiunga na Shule na ninaahidi kuyatekeleza kikamimifu.

KIJIJI/MTAA NINACHOISHI: ……..……
KATA…… TARAFA …..……
WILAYA …….. MKOA ……..

SANDUKU LA POSTA …… SIMU ……

SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI ……..

MISIMA SECONDARY SCHOOL

MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by Medical Officer in respect for Form I/V Entrants

Pupil's Full Name.....

Age.....

Blood cont (Red and White) .....

Stool: .....

Urinalysis: .....

Syphilis Test .....

T. B Test .....

Ears: .....

Chest .....

Spleen: .....

Abdomen: .....

ADDITIONAL INFORMATION: e.g Physical defects or impairments, infections. Chronic or family diseases etc.

.....

.....

.....

.....

I certify the above is fit/ unfit for admission into a secondary school

Designation: .....

Station: .....

Date: .....

Official Stamp: